

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MADINI

TUME YA MADINI

Telegramu "**MADINI**"
Simu: + 255-26 2320051
Nukushi: +255 26 2322282
Barua pepe:ceo@tumemadini.go.tz



S. L. P. 2292,
DODOMA

TAARIFA KWA UMMA

TOZO YA MRABAHA KWENYE GHARAMA ZA USAFIRISHAJI WA MAKAA YA MAWE KUTOKA KATIKA KAMPUNI YA TANCOAL

Kumekuwepo na taarifa za upotoshaji mkubwa ambazo zilichapishwa na Kampuni ya kuzalisha makaa ya mawe nchini TANCOAL kupitia tovuti ya www.miningreview.com tarehe 03 Septemba, 2019 na kusambazwa kwenye mitandao mingine ya kijamii.

Taarifa hizo zinadai kuwa Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini imeanza kuitoza TANCOAL tozo ya mrabaha kwenye gharama za usafirishaji wa makaa ya mawe kutoka mgodini hadi kwa mtumiaji wa mwisho wa ndani na nje ya nchi. Taarifa hiyo ikaendelea kudai kuwa, tozo ya mrabaha (asilimia tatu) na ada ya ukaguzi (asilimia moja) inatakiwa kuanza kulipwa mara moja.

Taarifa hiyo ikaendelea kueleza kuwa kampuni ya TANCOAL imelazimishwa kuuza makaa ya mawe kwa wateja wenye leseni za biashara ya madini hali itakayoongeza gharama za makaa ya mawe.

Tume ya Madini inapenda kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kifungu cha 87 (6) kinaelekeza namna ya kukokotoa mrabaha kwa kuzingatia thamani ya madini sokoni (kwa mtumiaji wa mwisho) ambayo inajumuisha gharama za usafirishaji hadi kwa mteja (Gross Value). Utaratibu huu wa malipo umekuwa ukifuatwa na kampuni nyingine zote zinazochimba ama kuuza makaa ya mawe isipokuwa TANCOAL.

TANCOAL imekuwa ikilipa tozo ya mrabaha kwa kuzingatia thamani ya madini yakiwa yadi ya Kitai bila kujumuisha gharama za usafirishaji kwenda kwa wateja. Pamoja na kuelimishwa mara kwa mara juu ya namna ya kukokotoa malipo ya mrabaha kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, TANCOAL imekuwa ikikaidi kulipa mrabaha kwa kuzingatia msingi huo.


Utaratibu ambao kampuni ya TANCOAL inautumia kwa kuwauzia wateja wa makaa ya mawe katika yadi ya Kitai badala ya kusafirisha wenyewe au kutumia wafanyabiashara wa madini walioidhinishwa (Mineral Brokers or Dealers) unakwenda kinyume cha Sheria. Kifungu cha 18 (1) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kinakataza mtu au kampuni yeyote isipokuwa mmiliki halali wa leseni ya madini au mfanyakazi wa wamiliki wa leseni hizo: kumiliki, kusafirisha au kuuza madini bila kuwa na kibali cha kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria.

Kutokana na Kampuni ya TANCOAL kulalamikia Madai ya Mrabaha inayotakiwa kulipa Serikalini, iliundwa Timu maalum kwa ajili ya kuhakiki deni la mrabaha unaojumuisha usafirishaji wa makaa ya mawe kwa kwa kipindi cha Septemba, 2011 hadi Juni, 2014 ambayo yalikuwa hayajalipwa pamoja na kufanya upembuzi wa madai ya mrabaha ambao TANCOAL inatakiwa kulipa Serikalini kwa kipindi cha Septemba 2011 hadi Juni, 2019.

Katika upembuzi na uchambuzi wa takwimu za mauzo na usafirishaji wa makaa ya mawe uliofanyika, imebainika kuwa TANCOAL inatakiwa kulipa USD 1,103,594 ikijumuisha na adhabu ya asilimia 50 kwa kipindi cha Septemba 2011 hadi Juni 2014. TANCOAL inapaswa kulipa USD 9,305,205 ikijumuisha na adhabu ya asilimia 50 kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Juni 2019. Jumla ya malipo ni USD 10,408,798 kwa kipindi cha Septemba, 2011 hadi Juni, 2019.

Tume ya Madini inaitaka kampuni ya TANCOAL kuacha kupotosha umma mara moja pamoja na kulipa madeni inayotakiwa kulipa kwa mujibu wa Sheria ya Madini na kanuni zake.

IMETOLEWA NA



Prof. Shukrani E. Manyi

KATIBU MTENDAJI

Septemba 16, 2019